JINA ........................................................................ NAMBARI ...................................

DARASA .................................................................... TAREHE ....................................

SAHIHI ....................................

102/2
KISWAHILI
OKTOBA 2019
MUDA: SAA 2 ½
KARATASI YA 2

# MTIHANI WA MWISHO WA MWAKA KIDATO CHA TATU 2019

*(Hati ya Kuhitimu Kidato Cha Secondari.(K.C.S.E)*

102/2
KISWAHILI
OKTOBA 2019
MUDA: SAA 2 ½
KARATASI YA 2

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

**MAAGIZO**

a) **Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu**

b) **Jibu maswali yote**

c) **Majibu yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa baada ya Kila swali.**

d) **Majibu yote yaandikwe katika lugha ya Kiswahili**

e) **Kijikaratasi hila kina kurasa kumi na mbili zilizopigiwa chapa.**

f) **Hakikisha kuwa maswali yote yapo.**

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|---|
| 1. | UFAHAMU | 15 | |
| 2. | UFUPISHO | 15 | |
| 3. | MATUMIZI YA LUGHA | 40 | |
| 4. | ISIMUJAMII | 10 | |
| | | 80 | |

## 1. UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Ulikuwa usiku wa manane. Maria hatawahi kuyasahau yaliyotokea usiku huo na madhara yaliyoikumba aila yake; ambayo hadi wa leo huwasumbua na kuwafuata kila waendako na hata kuishi. Matokeo ya kitendo kilichotekelezwa na nduguye mnuna yamesalia kama dondandugu moyoni mwake. Yeye hujaribu kuyafutilia mbali lakini yanakataa katakata kuondoka fuvuni mwake hasa anapomtazama nduguye mdogo.Tom, akitaabika bila miguu.

Maria alikuwa akidurusu somo la Fizikia Abdallah, kakake mkubwa akimpa Tom wosia " Tom, itakuwa bora ikiwa mtanena kwa amani na baba kuhusu tofauti zenu. Hamna haja ya kumrushia cheche za matusi. Kumbuka kuwa heshima kwa mzazi ni taadhima kwa mterehemezi. Matokeo yake ni baraka na **sudi** tele" Tom alikinai kuyatilia maanani mawaidha ya kaka yake. Akajitia hamnazo kudai kuwa baba yake amemdunisha kwa mwia mrefu na angemfunza adabu. Watu wote katika familia walijaribu kumsihi lakini ikawa kazi bure." upyaro haufai ndugu yangu. Hata kama una kimo kikubwa kuliko baba kumbuka kuwa ndiye mzazi aliyekulea wewe ", alidokeza Maria.

Baba yake Maria,Mugambi, alikuwa amechoshwa na vitendo vya mwanawe vya kutumia dawa za kulevya. Aghalabu Tom alikuwa akizua rabsha kila jioni baada ya kutoka shule.Mugambi alikuwa amemwadhibu mwanawe na hata kumshtaki katika kituo cha polisi lakini hakubalika. Watu walisema kuwa alikuwa na fedha nyingi kutokana na ulanguzi wa mihadarati. Jambo hili lilimwezesha kuhepa mitego ya askari kwa **kuzunguka mbuyu**. Tom akawa asiyesikia la mwadhini wala mteka maji msikitini. "Mzee ninataka unipe urithi wangu, la sivyo, leo utaiona dunia hii paa!"Tom akamtisha baba yake. Mugambi akaja juu na kumwambia mwanawe kuwa umri wake haukutosha kupewa urithi ingembidi akamilishe masomo kwanza, ajijengee msingi bora wa Maisha yake ya kesho na hata kupata mali yake mwenyewe." Mimi si mtoto. Ninataka uelewe kuwa leo ilikuwa siku yangu ya mwisho kuhudhuria shule, hiyo elimu ya wakoloni imenichosha! Katu sisomi tena,".

Akasema Tom. Punde si punde Mugambi alipandwa na za mkizi na kumwandama mwanawe kwa Makonde. Ikawa vurugu si vurugu **kuwamamanua** bila mafanikio. Licha ya kuumizwa na kujeruhiwa sehemu kadha za mwili wake, Tom alishikilia Kikiki na kuendelea kupambana na baba yake. Mama yake alipoona maji yamezidi unga, aliamua kuingilia kati na liwe liwalo. Kwa bahati mbaya Tom alimrushia teke la ubavuni na kumwangusha chini pu!

"Aghrr! haya yote unayotufanyia sisi wazazi wako yatakufuata daima" Achieng alilaani huku akigaragara sakafuni kwa maumivu tele" ninataka uniue leo, siwezi kulea kwa dhiki na taabu tele halafu unikosee mimi na mamako heshima namna hii utaona kilichomtoa kanga manyoya", Mugambi alimwambia mwanawe akiwa na uchungu mwingi moyoni. Majirani mimi nikiwemo walikuja kujionea sinema ya bure. "Teresia, unaona namna Tom alivyowakosea wazazi wangu heshima?" Maria aliniuliza." Kwa muda mrefu, familia yetu imekosa amani kwa sababu yako Tom kuzua fujo mara kwa mara. Amewajeruhi wazazi wangu mara nyingi huku akivunjavunja kenyekenye vyombo vya

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

mama.Tandabelua anaozua Tom hunifanya mimi na ndugu zangu kutohudhuria shule wakati mwingine. Huwa tunahofia kuangamizwa kwa wazazi wetu, hivyo kubaki nyumbani kama walinzi wao. Tom amegeuka hayawani.Hajali habali, "alinieleza Maria huku machozi yakimtirirka tiriri; njia mbilimbili. Nyumba yetu ilikuwa mita chache kutoka nyumbani kwa akina Maria. Nilikuwa wa kwanza kushuhudia Tom akiwatendea wazazi wake unyama pamoja na ndugu yake Abdallah. Alikuwa amewajeruhi vibaya. Abdallah alipojaribu kuwasaidia wavyele wake alirushiwa upanga uliompata barabara katika kisigino. Ninakumbuka namna Abdalla alivyochechemea kwa uchungu mwingi huku akiwa ameyauma meno. Kamsa ilivyotawala kwa mzee Mugambi. Watu wote walioshuhudia unyama wa Tom walilengwalengwa na machozi huku wakiulaani. Wanakijiji wa Umoja, waliamua kumpiga kitutu na kumfukuza. Alipotambua wamemzidi nguvu, alikimbia kiswara kuelekea upande wa chini. Kwa bahati mbaya, alianguka shimoni na kuvunjika miguu yote miwili. Aketipo na kudhukuru vitendo alivyokuwa akiifanyia familia yake, Tom hupatwa na mjuto mkubwa. Leo ameamini kuwa majuto ni mjukuu.

Maswali

a) Eleza msimamo wa Mugambi kuhusu kumpa mwanawe urithi ? (al.2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

b) Taja sababu kuu iliyomfanya Tom kutekeleza vitendo vya kinyama (al. 1)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

c) Eleza athari tano za Watoto kutowatii wazazi kwa mujibu wa taarifa hii. (al. 5)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

d) Kwa nini Tom aliepuka mkono mrefu wa serikali ? (al.1)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

e) Fafanua wasifu wa Tom kuligana na taarifa hii (al.3)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa (al.3)

i. Sudi ..........................................................................................

ii. Kuzunguka mbuyu ...........................................................................

iii. Kuwamamanua ...............................................................................

2. **UFUPISHO (ALAMA 15)**

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo

Kila walimwengu wanapotajiwa kuwa shambulizi la kigaidi limetokea mahali fulani, wimbi la taharuki huwakumba. Mashambulizi ya kigaidi yameongezeka katika siku za hivi majuzi ambapo kundi la watu linalohisi linaonewa na kukandamizwa huitumia mbinu ya kushambulia kwa kuvizia, hasa kutumia mabomu au kuteka ndege na kutishia kuilipua na wakati mwingine kuilipulia angani. Kuna mabomu yaliyotegwa na kulipuka katika maegesho ya magari au kwenye vizuizi vya magari. Mengine hutegwa na kulipuliwa katika afisi, mikahawa, makao ya watu, na kadhalika. Katika baadhi ya mashambulizi, wapo waliojitoa mhanga ambao hujilipua katika shambulizi.

Makundi ya watu wanaohasimiana ndio chanzo cha matendo ya kigaidi. Kundi linalohisi kuwa linaonewa au ambalo kweli linaonewa na ambalo ni dhaifu kuliko lile jingine, hufanya juu chini kushambulia kisirisiri. Nia ni kulipisha kisasi kwa jambo wanalohisi wamehiniwa, kuwa kundi hilo hudhani kuwa dhaifu halina njia wala uwezo wa kuyakabili moja kwa moja matendo waliyotendewa au wanayoendelea kutendewa, njia ya pekee, kwa maoni yao, huwa hii ya kushambulia kwa kushitukiza. Kiini cha uonevu kinaweza kuwa dini, uchumi, maamuzi ya kisiasa au jambo lingine lolote lile. Kinachobainika katika suala zima la mashambulizi ya kigaidi ni kuwa lipo jambo ambalo linazikera nyoyo za kundi fulani la watu walio wanyonge ambao huona kuwa njia ya pekee ya kudhihirisha hisia zao ni kupitia mashambulizi ya aina hii.

Mashambulizi ya aina hii ya athari zake nyingi. Kuna watu wanaouawa na wengine wengi kulemaa. Maisha ya watu hawa au jamaa zao wanaotegemea hubadilika na kujaa mvurugano uliokithiri. Kuna watoto ambao ndoto zao za kupata elimu zimetumbukia nyongo baada ya wazazi kuzikwa hai katika vifusi. Mbali na kukosa elimu na mahitaji mengine ya kimsingi, watoto hawa hupatwa na matatizo ya kisaikolojia baada ya kuona maafa yaliyowafika wavyele wao. Hata wale wanaosalimika kutoka kwenye vifusi hivi hawaishi kuandamwa na majinamizi yasiyoisha.

Mashambulizi ya kigaidi hayaathiri tu watu pamoja na kuharibu mali ya thamani ya lukuki ya pesa. Zipo athari nyingine hasi ambazo hudhihiri. Kwa mfano usalama wa nchi huwa mashakani. Wananchi wageni vilevile hujihisi kuwa dhaifu na dhalili katika nchi iliyovamiwa. Serikali husika hujikuta katika shutuma kwa kushindwa kutambua mipango hiyo mapema na kuzuia hasara ya nyoyo na mali. Aidha, jamii ya kimataifa huiona nchi hiyo kama yenye kukosa usalama na hivyo kuwaonya raia wake dhidi ya kuizuru. Iwapo nchi husika inategemea utalii kama kitega uchumi muhimu, basi hukosa wateja na waajiriwa katika sekta hii kupigwa kalamu.

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

Tatizo la ugaidi si la nchi moja au mataifa fulani mahususi wala hakuna nchi au taifa linaloweza kudai kuwa haliwezi kukabiliwa na tishio la kigaidi. Kuanzia Dar es Salaam, Nairobi hadi New York na London au hata Cairo hadi Riyadh na Baghdad, sote tunakabiliwa na tatizo hili hili. Hakuna ajuaye lini,vipi au wapi magaidi wamedhamiria kutekeleza unyama huu.

Labda swali la kujiuliza ni kwamba; je, upo uwezekano wa mwenendo huu huu wa kuwaangamiza watu, wengi wa wahasiriwa wakiwa wale wasio na hatia, kudhibitiwa na kumalizwa kabisa? Serikali za nchi mbalimbali zimejaribu kutumia uwezo wao wa kiuchumi na kiteknelojia ili kujaribu kuiondoa hali hii. Njia waliyoitumia ni mtutu wa bunduki ambapo makombora mazito yaliyogharimu pesa nyingi yanadondoshwa katika makao ya washukiwa. Hata katika hatua hii nayo, upo uwezekano mkubwa wa kuuawa watu wasio na hatia vile vile. Pia ni wazi kwamba uhasama na matokeo yake ni ulipizaji kisasi usioisha. Amani inakuwa nadra.

Juhudi za ulimwengu kulaani vitendo hivi ni nzuri ila hazitoshi. Utumiaji nguvu kutafuta ufumbuzi wa kitendawili hiki si suluhisho. Kama wanavyoeleza wanasosholojia, kila kitendo kina sababu hizo ndizo kichocheo cha vitendo vinavyojidhihiri. Hivyo basi jukumu lipo katika kutambua vichochezi vya mashambulizi na kujitahidi kuvitatua kwa njia ya kuleta usawa na usalama duniani.

Wapo watu wanaoona kuwa vitendo vya mataifa yaliyoendelea kwa nchi changa ndicho kilele cha ugaidi. Watu wanaona kuwa tabia ya mataifa hayo yenye uwezo kiuchumi na kiteknolojia kuamua na kudhibiti sera na Imani za nchi changa ni ugaidi uliokubuhu. Vikwazo hivi huwaacha viongozi hoi na wananchi kuteseka kufuatia ulazimishaji wa sera za kiuchumi na kisiasa zisizohusiana na mahitaji ya watu wanachi husika wala kuambatana na mahitaji ya nchi hizi. Hii ni hali inayoyatia mataifa yanayoendelea katika wasiwasi usioisha kutokana na dhiki zisizoisha kusababishwa na mataifa ya kigeni.

a) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 80, fupisha aya ya **pili, tatu** na **nne** (al.10,1ya mtiririko)

**Matayarisho**

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

**Nakala safi**

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

b) Eleza njia zinazotumiwa na mataifa ulimwenguni kupambana na ugaidi. (Maneno 40)

Al. 5,1 ya mtiririko

**Matayarisho**

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

**Nakala safi**

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

## MATUMIZI YA LUGHA

3 . (a) Taja sauti zifuatazo (alama 1)

i. Kikwamizo hafifu cha mdomo na meno.

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

ii. kiyeyusho cha kaa kaa gumu.

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

(b) Huku ukitoa mifano, onyesha miundo yoyote miwili ya silabi za Kiswahili (al. 2)

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

(c) Tunga sentensi iliyo na vipengele vifuatavyo:

iv. Kikanushi
v. Ngeli
vi. Wakati
vii. Kitendwa
viii. Mzizi
ix. Kiishio

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

b. Tumia kitenzi kishirikishi kipungufu bila kupoteza maana ya sentensi hii.

Mwanafunzi mmoja angali analala bwenini (al.2).

c. Onyesha miundo miwili tofauti ya ngeli ya U – ZI na utoe mfano kwa kila mojawapo (al.2)

d. Tunga sentensi moja kudhihirisha matumizi mawili ya kibainishi. (a.2)

e. Pikiwa ni kwa pika, ___________ ni kwa la huku gandamana ni kwa ganda na ______ ni kwa tua (al.2)

b. Andika sentensi ifuatayo upya katika wakati ujao hali timilifu.

Mucheru atangaza matokeo ya sensa. (al. 2)

i) Andika umoja wa sentensi ifuatayo katika hali yakinifu.

Kina mama wasingefika mapema fuoni, wasingewahi mashua.

j. Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa wingi.

Uso wa mtu huyu ulikuwa unatisha (al. 2)

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

k. Andika katika usemi wa taarifa. (al. 2)

"Nitakupa mali yako leo jioni," Mwekevu alimwambia Chandachema.

l. Tunga sentensi ukitumia kihusishi cha mtenda. (al. 1)

m. Bainisha matumizi ya "ki" katika sentensi hii.

Seremala a**ki**wasili atakuwa a**ki**tengeneza **ki**ti cha **ki**toto chake.

n. i. Eleza maana ya kirai. (al.1)

ii. Bainisha aina ya kirai kilichopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo. (al.1)

Mti mkuu ulianguka <u>kando ya mto.</u>

o. Ainisha vishazi katika sentensi: Endapo atanialika, nitamtembelea. (al. 2)

p. Onyesha shamirisho katika sentensi ifuatayo . (al.3)

Mwangeka alimbebea mkewe mzigo mwepesi kwa gari jipya

q. Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia kielelezo cha visanduku. (al. 4)

Mwanafunzi aliyesoma vizuri alipita mtihani wake

r. Andika kinyume cha sentensi ifatayo. (al.2)

For more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

- wasichana watano wanaingia darasani polepole.

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

s. Mkwezi hupanda miti ..................hufanya kazi maktabani, ..................hupanda mbegu shamb-ni, ........................ huendesha gari moshi na ........................ hubeba mizigo (al.2)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

4. **ISIMU JAMII**

Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Niaje wasee!Midterm ilibamba lakini ilikuwa fupi sana, tumerudi books, huu ni mwaka wa tatu tujikaze jo! Msifikirie hizo hepi zetu ni reality, kuchill ni jambo la maana jo! Ama niaje bro....hustle ni real, bidi ndiyo itatuokoa ya mabuku ni ngori.

Maswali

a. Tambua sajili inayohusishwa na kifungu hiki. (al.1)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

b. Eleza sifa zozote nne za kimtindo zinazojitokeza katika kifungu hiki. (al.5)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

c. Eleza sababu zinazosababisha matumizi ya lugha ya aina hii. (al. 4)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com